

## Usawiri wa Wahusika wa Kike katika Tamthilia za *Sudana* na *Dunia Hadaa*

John Mutua<sup>1</sup>, Rocha Chimerah<sup>2</sup> na Nancy Ngowa<sup>2</sup>

<sup>1</sup>Chuo Kikuu cha Machakos

<sup>2</sup>Chuo Kikuu cha Pwani

### Ikisiri

Suala la mahusiano ya wanawake na wanaume ulimwenguni limekuwa na linaendelea kuwafikirisha wahakiki na wanafasihi kote duniani kwa karne nyingi. Katika kuikabili kadhia hii, kumeibuliwa nadharia na mitazamo mbalimbali inayojaribu kueleza namna ya kuleta maridhiano ili kutuliza mgogoro baridi usiosita kwa kusudi la kutafuta usawa wa kijinsia. Mtazamo unaohusishwa na mhakiki wa kimarekani, Mary Ellman katika kitabu chake *Thinking about Women*, mwandishi huyo alielekeea kughadhabishwa na jinsi mwanamke alivyosawiriwa katika kazi zilizoandikwa na waandishi wanaume. Aidha, aliangazia jinsi baadhi ya waandishi wa kike wanavyoendeleza usawiri huo hasi wa wanawake katika kazi zao. Mawazo ya Ellman yaliungwa mkono na Millet (1970) katika *Sexual politics* alipowashambulia waandishi wa kiume kwa kuwasawiri wahusika wao wa kike kwa mtazamo hasi. Hali hii inachochea fikira kwamba waandishi wa kiume huwasawiri wahusika wa kike kwa namna tofauti wakilinganishwa na waandishi wa kike. Ikiwa kauli hiyo ina mashiko, basi itakuwa sawa kudai kuwa waandishi wa kiume ndio wa kulaumiwa kwa kuendeleza usawiri mbaya (hasi) kwa wahusika wa kike. Pia, ni sawa kudai kuwa waandishi wanawake wanawasawiri wahusika wa kike kwa mtazamo mzuri (chanya). Lengo la makala haya ni kulinganisha usawiri wa wahusika wa kike katika tamthilia ya *Sudana* ya Mazrui na Njogu (2006) na *Dunia Hadaa* ya Kisovi, (2007) ambazo zimeandikwa na waandishi wa jinsia tofauti. Makala haya yanakisia kuwa pana uhusiano wa karibu baina ya jinsia ya mwandishi na usawiri wa mhusika wa kike. Pia, tunachukulia kuwa pindi mitazamo ya waandishi hawa itakapobainishwa itasaidia kukadiria uwezekano wa fasihi kuwa chombo madhubuti katika kufikia usawa wa kijnsia. Ili kufikia lengo hili, tumeongozwa na nadharia ya Ufeministi wa Baada-ukoloni. Nadharia hii imetuwezesha kutambua sifa za mwanamke mwaafrika akisawiriwa na waandishi waafrika.

**Maneno Muhimu:** *chanya, mtazamo, mwanamke, ufeministi wa baada ukoloni, mhusika.*

### Utangulizi

Makala haya yanahusu uhakiki wa tamthilia mbili zilizoandikwa na waandishi wa jinsia mbili kwa kusudi la kulinganisha usawiri wa mhusika mwanamke. Msukumo uliopelekea uchunguzi huu umeelezwa katika sehemu ya usuli wa mada. Pia, nadharia ya Baada-ukoloni imefafanuliwa pamoja na uchanganuzi wa usawiri wa mwanamke katika tamthila za *Sudana* na *Dunia Hadaa*. Tumehitimisha kwa kutoa maeleo ya matokeo ya uhakiki kwa kuzingatia lengo la Makala.

### Usuli wa mada

Katika miaka ya hivi karibuni baadhi ya wahakiki na waandishi wa kazi za kifasihi kama vile; Ndungo (1985), Mbatiah (2001), Wamitila (2002) na Ntarangwi (2004) walipohakiki kazi zilizoandikwa kwa mwelekeo wa kifeministi wameanza kufikiri ya kwamba waandishi wa kiume huwasawiri wahusika wanawake katika kazi zao kwa njia tofauti ikilinganishwa na wanawake waandishi. Pia wanahisi ya kwamba, kwa kuwa kazi nyingi za kifasihi zimeandikwa na waandishi wa kiume, hiyo ndiyo sababu zimejaa taasubi ya kiume (Wamitila 2002, 2003). Mawazo yao yanaonekana kama mwangwi wa mawazo ya wafeministi wa kimagharibi kama vile Ellman na Millet. Ellman na Millet waliwashambulia waandishi wa kiume katika fasihi na kawashutumu kwa uwasilishaji wao wa wahusika wanawake katika fasihi.

Kwa mujibu wa Mbatiah (2001), wanawake wanaendelea kusawiriwa kwa mtazamo hasi katika fasihi iliyoandikwa na wanaume. Aidha, Ntarangwi (2000) alishadidia kauli hiyo na kuongeza kuwa waandishi wengi ni wanaume na kwa hivyo, mtazamo wa wanawake pamoja na tajiriba zao za maisha hazipo katika kazi nyingi za fasihi. Hili linadhahirika katika usawiri na uwasilishaji wa wanawake katika kazi za fasihi ambapo mtunzi ambaye aghalabu ni mwanaume, humsawiri mwanamke kulingana na tajiriba ya kiume na kama atamsawiri kwa mtazamo chanya hiyo huenda ikatokana na jinsi anavyomtarajia mwanamke kuwa. Labda hiyo ndiyo sababu wafeministi wa miaka ya sabini walisisitiza zaidi kazi zilizoandikwa na wanawake na zinazoeleza tajiriba ya mwanamke kama aijuavyo na aionavyo mwenyewe. Kwa hivyo, walihimiza na kupendeza zaidi kazi zinazopinga taasubi za kiume.

Kwa mujibu wa mawazo haya, mtafiti hana budi kujiuliza; Je, ni motisha gani inayompa mwandishi wa kiume hali ya kumsawiri mhusika mwanamke tofauti na mwandishi wa kike? Ama ni juhudzi za wanaume za kimakusudi kutaka kuwanyamazisha wanawake ambao wanawadhania kama kundi linalotishia usalama wao? Mwandishi wa Kifaransa, Simone de Beauvoir, katika kazi yake iitwayo *The Second Sex* (1949) alionekana kuwa na jibu la swalii hilo. Katika maandishi yake alionekana kuchukua mkabala wa kiharakti kwa kuzishambulia baadhi ya asasi zinazochangia kumdhahilisha au kumdunisha mwanamke katika jamii. Alizitambua asasi kuu tatu ambazo ni: ndoa, dini na utamaduni.

Aidha, bunge la taifa na Seneti nchini Kenya pamoja na mabunge ya kaunti (Majimbo) yalishirikisha idadi kubwa ya wanawake zaidi kuliko mabunge yaliyotangulia. Hili lilitekelezwa kuambatana na matakwa ya katiba iliyozinduliwa mwaka wa 2010 ambayo ilipendekeza ugatuvi wa mamlaka ya serikali. Kushirikishwa kwa asilimia kubwa ya wanawake katika nyadhifa za uongozi na uwakilishaji huenda kunaashiria taswira au mitazamo mipyä ambayo mtafiti anatarajia iakisiwe katika fasihi na hasa katika tamthilia zinazohakikiwa. Katika makala haya tumelinganisha tamthilia za waandishi wa kike na wa kiume; ya mwandishi wa kike ni *Dunia Hadaa* (Kisovi C.) na waaandishi wa kiume ni *Sudana* (Mazrui A.) akishirikiana na (Njogu K.) Hivyo, inakisiwa kuwa jinsia ya mwandishi inaathiri usawiri wa mhusika wa kike na pia mpito wa wakati huenda una mchango katika mabadiliko ya mitazamo ya kusawiri wahusika wa kike.

### Nadharia za Baada-ukoloni

Utafiti huu umeongozwa na nadharia ya Ufeministi wa Baada-ukoloni. Nadharia hii iliasisiwa kutokana na kazi ya Edward Said alipoandika vitabu vyake viitwavyo *Orientalism* (1978) na *Culture and Imperialism* (1993). Katika kazi zake alikosoa jinsi mataifa koloni ya Ulaya yalivyousawiri utamaduni wa nchi walizotawala au walizodhibiti katika enzi za utawala wao. Alidai ya kwamba mataifa hayo ya kimagharibi yalikuwa yakiutathmini utamaduni wa nchi walizotawala kwa misingi ya utamaduni wa kimagharibi bila kujali tofauti za tamaduni husika. Matokeo yake yalikuwa ni kuzidunisha na kuzidharau tamaduni za jamii walizotawala zikiwemo za Waafrika kwa kisingizio kuwa zilikuwa hazijastaarabika. Kwa maoni yao, kigezo cha ustaarabu kilistahili kukadirisha kwa misingi ya ustaarabu wa jamii za magharibi. Nadharia za Baada-ukoloni zinadai kuwa mtagusano wa kitamaduni baina ya mataifa tawala na mataifa tawaliwa ulisababisha athari kubwa katika mahusiano ya kijinsia.

Nadharia za Baada-ukoloni ni zao la jitihada na juhudzi ya kutaka kuzirekebisha hali fulani kuhusu jinsi mataifa ya kimagharibi yanavyoziangalia nchi zilizokuwa koloni zao. Harakati za kuuyanya mwelekeo huu zilianza miaka ya 1950 wakati ambapo Ufaransa ilikuwa ndio kwanza inaacha uhusiano wake na Indochina, wakati wa vita vya ukombozi wa Algeria, vuguvugu la Maumau nchini Kenya pamoja na kuondolewa mamlakani kwa Farauk aliyekuwa mfalme Misri. Kwa mintarafu hiyo, tunalinganisha usawiri wa wahusika wa kike kwa mtazamo wa waandishi wa jinsia tofauti.

Ufeministi wa baada-ukoloni unajitenga na mfumo mzima wa ufeministi wa kimagharibi na kuushutumu kwa kutojihuisha na suala la kijinsia na badala yake kuegemea upande mmoja wa wanawake na kuwabagua wanaume. Aidha, waitifaki wa Ufeministi wa Baada-ukoloni wanajihuisha

na mambo kadha: Kwanza, wanapinga ujumuishaji au ubia katika masuala ya wanawake duniani kote. Wanaamini ya kwamba mfumo wa ufeministi wa jumla unapuuza masuala yanayowakumba wanawake weusi na wasio wa asili ya magharibi. Pili, wanaamini ya kuwa masuala yanayowahusu wanawake ni tofauti kutegemea utamaduni wao na taifa wanamoishi. Tatu, wanashutumu wanawake wa magharibi kwa kuwa ‘kinywa’cha wanawake wote ulimwenguni. Mwisho, ufeministi huu unatoa nafasi ya kujadili masuala ya wakati wa ukoloni kama vile uhamiaji, utumwa, ukandamizaji, ukinzani, ubaguzi wa rangi, ubaguzi wa kijinsia, makazi na shinikizo za mataifa ya kimagharibi kwa mataifa yanayoendelea. Nadharia za Baada-ukoloni hazipingo ufeministi wa kimagharibi lakini zinapendekeza nadharia zote za kipindi cha baada-ukoloni zihusishe na masuala ya jinsia pasipo kupendelea upande mmoja.

#### **Usawiri wa wahusika wa kike katika *Sudana***

Wahusika wa kike wamesawiriwa kwa namna mbalimbali katika tamthilia ya *Sudana*. Sifa zilizobainishwa ni pamoja na mwanamke kutazamwa kama mkombozi kama inavyodhihirika katika sehemu ya utangulizi wa tamthilia hii. Mhusika Sudana anasawiriwa kama mkombozi wa watu waliokandamizwa kisiasa na kijisia. Mathalani, katika shairi lake aliowaandikia wanawe (Waafrika) kote barani Afrika na kokote ulimwenguni akiwahimiza wakutane ili kujadili matatizo yanayolikumba bara lao kwa nia ya kupigania ukombozi wa nchi zao. Ubeti ufuatao unasema;

Wanangu, wana-Afrika,  
Karne nenda, karne rudi  
Silaha mikononi... (Uk.3)

Anawahimiza waungane, wapigane na makabila yanayowatesa. Anahamasisha kila mmoja ajitoe mhanga kupinga unyanyasaji na udhalimu unaoendelezwa na mabeberu katika mataifa mbalimbali ya Kiafrika. Kadhalika, anawapongeza wanawe waliofaulu kupigania ukombozi wa nchi zao katika mataifa kama vile Kenya, Guinea na Algeria. Anawashauri wengine kutumia ujasiri uo huo ili kupigana dhidi ya udhalimu katika nchi zinazoendelea kunyanyaswa.

Na huko Kenya  
Huko Guinea, na Algeria  
Mlijichoma dhidi ya ubeberu mkapambana nao  
Kwa midundo ya kuchoma (uk.3-4)

Vita hivyo vilisababisha kifo cha mwanawe msaliti, Sudzungu. Kifo chake kinaashiria kuondolewa kwa kizazi kisichoensi wanawake katika jamii. Kizazi hicho ni cha wasaliti ambao huchelewesha ukombozi wa wanawake na Wazanji (Waafrika). Baadaye hofu inawakumba Amerigo, Muzungu na Wamerope ni ishara kuwa dhuluma dhidi ya waafrika na wanawake inafikia kikomo. Aidha, watoto wake wanapokufa, damu yao inaibia ari kubwa ya Sudana kupigania ukombozi wake (mwanamke) na wa waafrika.

SUDANA: ...  
Ndiyo, katika kifo chako  
katu hutakufa Sizwe;  
Kwani katika kifo chako  
mna mbegu zisizo idadi... (uk.40)

Sudana anapigana kwa jino na ukucha ili kuepuka kunyanyaswa kimpenzi na Amerigo na pia kuwatetea wanawe wanaoteswa na kuuawa na wazungu. Anawapongeza na kuwaunganisha waafrika waliotawanyika kote ulimwenguni akiwahimiza wawe na umoja ili wapiganie ukombozi wa nchi zao. Usawiri huu unaafikiana na yale nadharia za Baada-ukoloni zinavyosisitiza. Nadharia hizi zinapendekeza kujadiliwa kwa dhuluma za ukoloni kwa mataifa ya Kiafrika kwa sababu katika utawala wao wanawake walidhulumiwa mara mbili. Kwanza, waliteswa kama waafrika na pili kama wanawake.

Mhusika Sudana pia amechorwa kama mwanamke shujaa. Ushujaa wake umejitokeza kwenye makabiliano yake na Amerigo. Amerigo anapajaribu kumkumbatia, Sudana anajitatua na kumpiga

meno shingoni mpaka anapiga usiyahi na kumwacha. Alimkashifu kwa kutoweza kupambanua baina ya ‘ngarawa’ na ‘kidau’. Hakujali kuwa wakati huo alikuwa mateka na mhitaji msaada wa Amerope. Tamko lake linamsawiri kama shujaa.

SUDANA: Unahodha wako na mashua kubwa Atlantini haufui dafu kwa ngarawa hii Bahari-Zanjini.

AMERIGO: (*Kwa hofu*) **oh my God! Easy, dear, Easy.** Haya basi! Basi! Yamekwisha. Usicheze na upanga tafadhali. Hebu uweke kando (*Anarudi kinyumenyume kuelekea mlangoni*). ...” (uk.27)

Hatua yake ya kukataa kushiriki mapenzi na nahodha mkuu wa AMEROPE ni ishara ya ushujaa wake. Aidha, halegezi msimamo wake baada ya kutiwa hofu na Amerigo kuwa maisha ya mwanawewe Shume yalitegemea ushirikiano wake na Wamerope. Sudana anajijasirisha kumshutumu na kumtukana Amerigo kutoptana na azima yake ya kumbaka.

SUDANA: (Kwa hasira) Usiniguse! Usiniguse! Hayawani we! Usijaribu kunigusa mie! (uk.37)

Kitendo cha Sudana kumng’ata Amerigo hadi anapiga usiyahi kinaweza kufasiriwa kama ushujaa wa mwanamke kujitetea dhidi ya dhuluma za wanaume. Mwandishi anaeleza:

(*Anamkamata mkono Sudana kwa ghafla. Anamshika na kujaribu kumkumbatia. Sudana anajaribu kujitatua; mwishowe anampiga meno shingoni Amerigo.*) (uk.25)

Uhusiano wa Amerigo na Sudana unadhihirisha sifa ya kijasiri na ushujaa wa Sudana (Mwanamke).

Sifa ya ushujaa wa mwanamke haiwezi kutambuliwa kwa kuongozwa na nadharia inayobagua kama zilivyo nadharia za ufeministi wa kimagharibi unaomsawiri mwanamume kama adui wa mwanamke. Mtazamo wa ufeministi wa Baada-ukoloni unahimiza usawa wa kijinsia. Kauli hii ni sawa na maana ya methali, ‘Mgala muue na haki umpe.’ Bali na unyonge wa mwanamke kama binadamu yejote, akistahili sharti apewe.

Mwanamke amesawiriwa kama mpiganiaji haki za wanawake. Sudana anahimiza umoja wa wanawake kote ulimwenguni ili kupambana na udhalimu dhidi yao unaowanyima haki zao. Msomaji anahisi kwamba ukombozi anaodhamiria Sudana sio tu kutoptana na dhuluma za wanaume kwa wanawake lakini pia dhuluma dhidi ya Waafrika (Wazanji). Anawahimiza kupigana na changamoto zinazowakibili kama watumwa wa wakoloi na pia kunyanyaswa kama wanawake bila kutamauka. Vivyo hivyo, Sudana anatamani na kuitazamia siku ambayo wanawake wote watavunja pingu za udhalimu na kujiweka huru. Huu ndio ujumbe unaopatikana kwenye shairi hili:

Ni lini milima hii  
Ya dhuluma,  
Ya watu kudhulumiwa,  
Itakapoyeyuka  
We koja za asumini?  
Ni lini umoja wa hisia zetu  
Utatufungulia ukurasa wa utulivu? (uk.28)

Vifo vyta wanawe wawili Shume na Sudzungu havimtishi wala kumkatisha tamaa, badala yake anapata ari zaidi ya kuzidisha mapambano ya kutetea haki za wanawake wanaonyanyaswa kote ulimwenguni. Katika shairi hili Sudana amechorwa kama mpiganiaji haki mwenye uwezo wa kuwaunganisha watu wengine ili kufanikisha juhudhi za mapambano. Wito wake unaungwa mkono na watu wengi wenye ari hiyo ya kupigania haki. Mwandishi anamsawiri kama mwanaharakati shupavu katika upiganiaji haki za wanawake.

SUDANA: (*Kwa sauti dhabiti*)  
Usisahau jina lako Shume!  
Wakati ni wetu Shume  
na kifo chetu,

ni njia tu  
katika maisha yetu ya milele.  
(*Anainua ngumi*)  
Mapambano yaendelee!

SAUTI NYINGINE: (*Kwa ndani*) Mapambano yaendelee!  
SUDANA: Mapambano yaendelee! (uk.54)

Licha ya waandishi kujitahidi kuonesha ushindi wa mhusika wa kike dhidi ya dhuluma anazofanyiwa na mwanamume, ni kinaya kuwa hatimaye mwanamke anasawiriwa kama mshinde. Baada ya juhudhi nyingi alizofanya Sudana kupinga kunajisiwa na Amerigo, hatimaye Amerigo anaonekana kufanikisha shabaha yake ingawa bila hiari ya Sudana. Sudana alisawiriwa kama mwana mke jasiri, mwenye msimamo thabiti na usiroyumbishwa na kila namna ya ushawishi na vitisho. Mwandishi anapoonyesha kufanikiwa kwa juhudhi za Amerigo kumbaka Sudana baada ya kuzirai, msomaji anapata wazo la kushindwa kwa mwanamke na kufaulu kwa mwanamume.

Amerigo: lo! hii ndiyo nafasi yangu!  
Nikiikosa pengine nitaruka patupu! Mungu kweli ni karimu!  
Amenirahishishia mambo! ... (uk.44)

Sudana akiwa mhusika mkuu, anasawiriwa na waandishi kama mwanamke shupavu na mshindi katika harakati za kupinga dhuluma dhidi ya wanyonge na pia wanawake. Sudana anaelekea kuibuka mshindi katika vita dhidi ya unyanyasaji unaoendelezwa na Wamerope kwa Wazanji na pia, anakaribia kumshinda Amerigo katika juhudhi zake kutaka kumnajisi. Msomaji anastaajabishwa na tukio la mwisho ambapo mwandishi anamkatisha mwanamke matumaini ya kuwa mshindi na badala yake kumgeuza mshinde. Mhakiki anashangaa ni kwa nini mwandishi hakutaka mwanamke anyakue ushindi hata baada ya kumtarayisha kushinda udhalimu dhidi yake na Wazanji wenzake. Hatimaye Sudana anabakwa baada ya kupigana kwa jino na ukucha. Jambo hili linamporomosha mhusika wa kike na kumfanya aonekane mshinde. Kufanikiwa kwa Amerigo na kushindwa kwa Sudana ni usawiri hasi wa mwanamke. Kwa hivyo, katika kumjenga mhusika mkuu, Sudana, mwandishi anadhihirisha mtazamo hasi kwa wahusika wa kike.

#### **Usawiri wa Mwanamke katika *Dunia Hadaa***

Mwandishi wa tamthilia ya *Dunia Hadaa* ni Catherine Kisovi. Huyu wandishi wa kike ambaye amemsawiri mhusika wa kike kwa namna mbalimbali. Alimpa mhusika wa kike sifa nyingi hasi akilinganishwa na waandishi wa Sudana. Sifa hizo zilidhihirisha mtazamo wa mwandishi huyo kuhusu mwanamke. Zifuatazo ni sifa na dondoo za mazungumzo zinazothibitisha usawiri huo.

Mwanamke amesawiriwa kama aliyeshindwa na jukumu la ulezzi. Aghalabu jukumu la ulezzi wa watoto linatazamiwa liwe la wazazi wote wawili (mzazi mwanamke na mwanamume). Hata hivyo, sivyo ilivyo katika baadhi ya jamii za Kiafrika. Katika tamaduni nyingi za kiafrika mtoto anapokuwa wa kike, wajibu wa kumlea na kumwadilisha hukabidhiwa mamake na wala sio mwanamume (babake). Vivyo hivyo, mtoto wa kike anapoharibika kitabia atakayelaumiwa ni mamake (mwanamke). Kwa mintarafu hiyo, Bi. Ruzuku mamake Hasada anakabiliwa na jukumu hilo la kijamii la kumlea na kumwadilisha bintiye. Aidha, jukumu hilo linaonekana kumshinda na matokeo yake ni majuto kwake na jamaa yake. Bi. Ruzuku anaishia kulalama tu. Katika dayolojia ifuatayo hali hiyo inajitokeza:

BI. RUZUKU: (Akimkatiza) Basi ninafikiria kwamba wewe u mionganoni mwa wasio na akili na ...

HASADA: Mama unaweza kunitusi namna hiyo?

BI. RUZUKU: Mwana, nitakulea hadi lini? Sasa wewe ni mtu mzima na una nyumba yako. Unasumbuliwa na nini?

HASADA: Kwani nimekwambia unilee? Mimi nina mume na watoto. Ikiwa utanilea, nao watoto wangu watalelewa na nani? (uk.61)

Matamshi haya yanadhihirisha kushindwa na kutamaushwa kwa mama mzazi kuhusu tabia za bintiye asiyembilika wala kusemezeka. Kufokeana kwa mama na bintiye ni ushahidi wa utovu wa

hesima na adabu wa Hasada kwa mamake. Jambo hili linamjenga Bi. Ruzuku kama mama aliyeshindwa kutimiza matarajio ya jamii yake kuhusu wajibu wake wa kumwadilisha bintiye. Mazungumzo yafuatayo yanadhihirisha utamaushi wa Bi Ruzuku khusu kumrudi bintiye.

BI. RUZUKU: (*Anawasha jiko na kuanza kuandaa kiamsha kinywa*) Huyu mtoto wangu sijui ana nini? Kutoka kwa mumewe juzi tu na hatulii hapa. Hii ni tabia gani? Sijui nilishindwa wapi? Nikiambiwa na babemtu kuwa toto lenyewe naliendekeza sana, nikipinga. Sasa najua mchelea mwana kulia hulia yeye. Najuta sana hata ingawa majuto ni mjukuu. Nifanyeje! (uk.57)

Bi. Ruzuku anakiri kuwa yeye ndiye anayestahili kulaumiwa kwa kumdekeza bintiye licha ya kutahadharishwa na mumewe dhidi ya kufanya hivyo. Baadaye anajutia kushindwa kwake. Yeye haonekani kama mama aliyefaulu katika ulezi na hasa kustahili kuheshimiwa na bintiye anayeonekana kumwagiza amtengenezee kiamsha kinywa. Kwa upande mwengine, Hasada amesawiriwa kama mtoto asiyetii na kumheshimu mzazi wake. Utamaduni wa baadhi ya jamii za kiafrika wa kumlaumu mzazi wa kike kwa kuzembea la ulezi wa binti ni suala ambalo haliwezi kueleweka kwa misingi ya ufeministi wa kimaghari ambao huupuza changamoto zinazowakabili wanawake waafrika. Ufeministi wa Baada-ukoloni unahimiza masaibu ya wanawake waafika yachunguzwe kwa jicho la kiafrika bila kujumuishwa na ya wanawake weupe. Hii inatokana na tofauti ya mazingira wanamoishi.

Mwanamke pia amesawiriwa kama kifaa cha kutekelezea uovu. Mwandishi amewatumia wanawake wawili, kila mmoja kwa zamu yake ili waivunjeunje ndoa ya Nora na Matemo. Sababu zao za kuiharibu ndoa hiyo zinachochewa na roho ya chuki, wivu na ari ya kutenda uovu. Hasada hampendi wifiye kwa madai kuwa ni mnyamavu na anaringa kwa kuwa ana elimu. Mwandishi anamtumia ili kupalilia chuki baina ya Nora na Matemo. Anazua ugomvi kwa kumwandikia nduguye Matemo barua na kumpigia simu ya kuchochea uhasama baina ya mke na mume. Hatimaye anafaulu kusababisha Nora kutilikiwa na mumewe Matemo. Talaka hiyo inafungua nafasi kwa mwanamke mwengine (Anasa) kuisambaratisha familia hiyo. Dondoo hili linadhihirisha chuki na uovu uliomjaa mhusika wa kike.

HASADA: (*Akiangua kicheko*) Aa... aa... aii...luuuu. Mama, nani mwengine? Sasa ni hivi, niliwasiliana kwa simu na Matemo leo ii hii na tukasema mengi. Nimewaandikia barua wakiwa na huyo bibi yake. Sijui kama baada ya kuiapata na kuisoma huyo wifi atakuwa na usalama popote.

BI. RUZUKU: Ati unasema nini? Ni kwa nini asiwe na usalama popote?

HASADA: Baada ya Matemo kuisoma barua hiyo, macho yake yatafunguka na Ataona mbali. (uk.64)

Mwandishi anamtumia Anasa ili kumwadhibu Matemo kwa kumtaliki na kuitelekeza jamaa yake. Anamsawiri kama mwenye vitendo vinavyochukiza na kumdhailisha kitabia. Ni mlevi, anatoka nje usiku akiandamana na rafikiye Makuruhu licha ya kuwa ana mpango wa kufunga ndoa na Matemo. Anamwacha Matemo nyumbani na kuandamana na mpenziwe pasipo kujali hisia za Matemo ambaye amekwisha kumtaliki mkewe ili afunge ndoa naye. Anasa anaporudi keshoye, hana heshima kwa wazazi wa mumewe na anatapika kitandani na kutisha kufanya haja zote kitandani humo. Mazungumzo yafuatayo yanadhibitisha hayo:

MATEMO: Hayo tutayajua. Mbona unanuka pombe?

ANASA: Kuna nini hata nikilewa? Nini cha mno? (*Anaingia na kujitupa kitandani. Baada ya dakika chache Matemo anamfuata katika chumba cha malazi*)

MATEMO: (*Kwa mshangao*) Ala! Una nini wewe mwanamke? Unatapikia kitanda na kutema mate sakafuni bila kujali? (uk.94)

Matamshi ya Anasa yanadhihirisha upungufu mkubwa wa maadili. Inaonekana kana kwamba wahusika hawa; Hasada na Anasa wametumiwa na mwandishi kama kifaa cha kutekeleza adhabu ambayo mwandishi alinuia kumpa mhusika mwanamume ambaye amefanya makosa katika uhusiano wake na mkewe katika ndoa.

Wahusika hawa wamechorwa kama viumbe waliojawa na tamaa kubwa ya kuharibu, chuki na kisasi. Mhakiki anahisi kuwa kuna njia mbadala za kutekeleza adhabu hiyo bila kuwatumia wahusika wa kike kwa namna inayompa msomaji taswira hasi kuwahuusu. Kwa mfano, kuhusisha mashauriano na mazungumzo mbele ya wazee wao ama hata kufuata mkondo wa sheria za dini au nchi. Kumtumia mhusika wa kike kwa namna hiyo kunamfanya aonekane kama kifaa cha kuadhibia. Hali hii inawakilisha mtazamo hasi wa mwandishi kuwahuusu wahusika wa kike.

Mwanamke si mwaminifu katika ndoa. Mwandishi kupitia kwa mhusika Sidi anatujuza kuwa, kuna siku mkewe hufika nyumbani jogoo la kwanza. Jambo hili humtitia wasiwasu mume wake ambaye hamtaraji mke wakeachelewe hadi kufika nyumbani usiku wa manane. Sidi anaeleza kuwa mara kwa mara mkewe hufika nyumbani akiandamana na jibaba lenye gari na humbusu kabla ya kumuaga mbele ya mumewe (Sidi). Tabia hii ya kukosa uaminifu na kutojali katika ndoa ndiyo inayompelekea mumewe kufikia uamuzi wa kumtaliki. Huu ni ukosefu wa uaminifu katika ndoa kama inavyodhahirika katika mazungumzo yafuatayo:

SIDI: "...Nilikuwa na wasiwasu sana. Mara tu nikasikia mlion wa gari, kuchungulia dirishani, nikalionia jibaba lenye tumbo kama kiriba limesimamisha gari. Likambusu mke wangu. Kuona hayo sikuweza kuvumilia..." (uk.74)

Ukosefu wa uaminifu katika ndoa hasa kwa mwanamke ni jambo ambalo halitarajiwi katika jamii nyingi za Kiafrika. Pale linapotokea mwanamke hujipotezea heshima yake katika ndoa. Aghalabu mwanamke anapokuwa na tabia hii huficha ili angalau mumewe asijue. Ikiwa anaonesha hadharani kama alivyofanya mkewe Sidi, basi huyo atakuwa amekia mipaka. Tendo la mkewe Sidi lina msawiri kama aliyekosa uaminifu katika ndoa. Mwandishi anaonyesha mtazamo hasi kwa wanawake kupitia mhusika huyo. Usawiri huu unaoana na kile ambacho nadharia ya ufeministi wa Baada-ukoloni inachokitaja kama athari ya mtagusano wa baadhi ya mataifa tawala na mataifa yaliyotawaliwa. Mtazamo wa kuwatweza na kuwahusisha wanawake na uovu unaonekana kama ulioigwa kutoka kwa wakoloni. Mwandishi wa tamthilia hii yamkini anaendeleza mawazo ya kasumba ya ukoloni ambayo jamii yake ilirithi enzi za ukoloni mkongwe.

Pia mwanamke amechorwa kama mwenye fadhila. Chudi bintiye Matemo anaonekana kumjali mamake kwa kila jambo. Anamjengea mamake (Nora) nyumba na kumnunulia gari na anahiari kumwajiri dereva wa kumwedeshea gari hilo. Hii ni fadhila kubwa kwa mtoto ye yeyote kwa mzazi wake. Ingawa watoto wa kike wa Nora wamesawiriwa kwa njia chanya hapa, msomaji anahisi mwandishi amefanya hivyo kimakusudi ili asisitize hasara aliyopata baba yao Matemo kwa kutoiwajibikia familia yake. Mazungumzo yanayofuata yanadhihirisha hayo.

CHUDI: Hata! Ikiwa hujasahau kuendesha gari utajiendeshea lakini kama umesahau, nitakuajiria dreva atakayekupeleka kokote unakotaka.

NORA: Nitahiari kujidoresha. Ahsante.

CHUDI: Mama, nina mpango wa kukujengea kasri. Wataka jumba la ghorofa au la kawaida? (Uk.98-99)

Yamkini mwandishi anawasawiri mabinti wa Matemo wakiwa na shukrani ili aoneshe jinsi baba yao alivyofaa kujuta apatapo habari ya ufanisi wa iliyokuwa familia yake. Ama hii ni mbinu ya mwandishi kulinganua maisha ya watalaka hao wawili. Hata hivyo, tunapata taswira ya wahusika wa kike walio na shukrani kwa mzazi aliyekumbana na mateso mengi katika ulezi wa watoto. Usawiri huu unawakilisha mtazamo chanya kuhusu wahusika wa kike katika kazi ya mwandishi husika. Usawiri huu unaelekeea kuchochewa na kile nadharia ya Baada-ukoloni inachodai ni juhudzi za kimakusudi za baadhi ya waandishi kutaka kuirekebisha hali fulani ya mahusiano ya kijnsia ambayo wanahisi ilisababishwa na hali ya baadhi ya mataifa ya magharibi kuutathmini utamaduni wa waafrika kwa kutumia vigezo vyao. Nadharia hii inapinga juhudzi zozote za kuutathmini utamaduni wa kiafrika kwa kutumia mizani ya utamaduni wa kimagharibi.

### **Hitimisho**

Ulingenishaji wa usawiri wa wahusika wa kike katika tamthilia za *Sudana* na *Dunia Hadaa* umeonesha kuwa, nanma mhusika wa kike atakavyosawiriwa katika kazi za fasihi una uhusiano wa karibu na jinsia ya mwandishi wa kazi husika kwa kiwango fulani. Uhakiki wa tamthilia ya *Sudana* ilioandikwa na waandishi wa kiume imeonesha taswira tofauti ya mhusika wa kike na tamthilia ilioandikwa na mwandishi wa kike. Katika *Sudana*, waandishi wamebainisha sifa nyingi chanya kwa mhusika wa kike. Kwanza, wamesawiriwa kama viongozi wa ukombozi sio tu wa nchi zao bali pia walio tayari kuikomboa jinsia ya wanawake kwa jumla. Pili, wamesawiriwa kama mashujaa kwenye vita vyta kuwaondoa wakoloni katika nchi zao za kiafrika. Tatu, wamesawiriwa kama wapiganiaji haki za wanawake dhidi ya kudhalilishwa na wanaume. Mwisho, wamechorwa kama wahusika walioshindwa kutimiza ndoto zao licha ya juhudhi nyingi walizowekeza katika harakati za ukombozi. Kufungamana na usawiri huo, tunaweza kudai kuwa waandishi wa kiume katika tamthilia ya *Sudana* wamewasawiri wahusika wa kike kwa mtazamo unaopendeza (chanya). Usawiri huo unaonekana kuafikiana na madai ya nadharia ya ufeministi wa Baada-ukoloni. Kwa mujibu wa nadharia hii, hali ya kumsawiri mhusika mwanamke kwa mtazamo hasi ni mojawapo ya athari ya mtagusano wa waafrika na mataifa ya kikoloni yaliyowadhibiti kisiasa kabla ya uhuru. Waandishi wa tamthilia ya *Sudana* wanawawiri hali tofauti na hiyo kama mbinu ya kurekebisha kosa ambalo yamkini ilitokea katika enzi za kikoloni.

Hata hivyo, hali tofauti na hiyo inadhihirika katika uhakiki wa *Dunia Hadaa* ilioandikwa na mwandishi wa kike. Katika tamthilia hii, mhusika wa kike ameoneshwa kama aliyeshindwa na jukumu la ulezi, amesawiriwa kama kifaa cha kutekelezea uovu na pia amechorwa kama mtu asiye mwaminifu katika ndoa. Hii ni thibitisho kwamba katika tamthilia ya *Dunia Hadaa*, mwandishi amemsawiri mhusika wa kike kwa mtazamo mbaya na usiopendeza (hasi). Ulingenishaji wa usawiri huo unathibitisha ya kwamba waandishi wa kiume huwasawiri wahusika wa kike kwa mitazamo tofauti wakilinganishwa na waandishi wanawake katika tamthilia husika.

Tofauti za kimtazamo katika usawiri wa wahusika wa kike unaobainika katika uhakiki wa tamthilia hizo mbili ni kiwakilishi cha namna jamii inavyolichukulia suala la mahusiano ya kijinsia. Fasihi kwa jumla inajibainisha hapa kama chombo cha kutathminia mawazo, itikadi na mielekeo ya watu kwenye masuala yanayoiathiri jamii husika kwa kupitia sanaa. Kwa mintarafu hiyo, fasihi inaakisi mabadiliko ya mitazamo kama ilivyo katika kipindi maalumu cha wakati na pia kubashiri matarajio yake katika siku za baadaye. Tamthilia ya *Sudana* imeonesha mabadiliko ya taswira ya mwanamke yanayohusishwa na waandishi wa kiume.

Kwa upande mwingine, mwandishi wa kike haoneshi kubadilisha mtazamo wake kiwakati kama inavyotarajiwa. Taswira inayodhihirika katika *Dunia Hadaa* ni ya mwanamke anayekwaza maendeleo ya mwanamke mwenzake na hivyo kuendelea kuwaonesha waandishi wa kike kama wanaochangia kifasihi kuchelewesha ukombozi wao kwa usawiri unaokosa matumaini. Suala hili linaonekana kutinga juhudhi za waandishi wa kiume kuitumia fasihi kama chombo cha kumkomboa mwanamke. Aidha, waandishi wa kiume hawawezi kulaumika kwa kiwango kikubwa kwa kuendeleza usawiri hasi wakilinganishwa na waandishi wa kike. Ingawaje mabadiliko huja kwa hatua kama inavyodhihirishwa na waandishii wa kiume, waandishi wa kike wanaonekana kulemewa na kasumba ya kikoloni inayowadunisha wanawake. Mtazamo huu unaafikiana na madai ya nadharia ya ufeministi wa baada-ukoloni. Nadharia hii inahusisha usawiri hasi wa wanawake na athari ya mtagusano wa wakoloni na waafrika katika enzi zao barani Afrika. Hata hivyo, jamii inaonesha mabadiliko ya kimtazamo wa usawiri wa mhusika wa kike. Yamkini mabadiliko haya yamechochewa kisiasa kama ilivyobainika kikatiba na kudhihirika kifasihi kupitia waandishi wa kiume.

### **Marejeleo**

De' Beauvoir, S. (1949), *The Second Sex*. Pan books publishers.

Ellmann, M. (1968), *Thinking about Women*. Brace & World Publishers.

Kisovi, N. (2007), *Dunia Hadaa*. The Jomo Kenyatta Foundation.

- Kenya Constitution, (2010), *Representation of the people*. Government Printer
- Mazrui, A. & Njogu, K. (2006), *Sudana*. Longhorn Publishers (K) Ltd.
- Mbatiah, M. (2001), *Kamusi ya Fasibi*. Standard Textbooks Graphics & Publishing.
- Millet, K. (1970), Sexual Politics. Doubleday OCLC 489817513.
- Ndungo, C. (1985), Wanawake na Mabadiliko ya Kihistoria Katika Kiswahili. (Unpublished Master's thesis). University of Nairobi.
- Ndungo, C. (1993), *The Image of a Woman in African Oral Literature: Case of Gikuyu Oral literature*. (Unpublished PhD thesis). Kenyatta University.
- Njogu, K. & Chimerah, R. (1999), *Ufundishaji wa Fasibi, Nadharia na Mbinu*. Jomo Kenyatta Foundation.
- Ntarangwa, M. (2004), *Uhakiki wa Kazi za Fasibi*. Rock Island, IL 61201.
- Said, E. (1993), *Culture and Imperialism*. Vintage Books.
- Said, E. (1978), *Orientalism*. Pantheon.
- Wamitila, K. (2002), *Uhakiki wa Fasibi, Misingi na Vipengele Vyake*. Phoenix Publishers Ltd.
- Wamitila, K. (2003), *Kamusi ya Fasibi, Istilabi na Nadharia*. Focus Books.
- Wafula, R. & Njogu, K. (2007), *Nadharia za Uhakiki wa Fasibi*. The Jomo Kenyatta Foundation.

